

MUUNDO WA KANISA LA KRISTO.

Mwandishi – John Grubb

Kanisa ni Ufalme ambao Kristo anatawala juu yake kama mfalme (1 Tim. 6:15; Yoh. 18:37). Wakristo ni raia wa Ufalme huu (Kol. 1:13; Ebr. 12:28; Ufu. 1:19). Ulimwengu ni mahali ulipo Ufalme huu (Mt. 28:19; Mk. 16:15; Mdo. 1:8). Kuzaliwa upya ndiyo njia ya kuingia katika Ufalme huu (Yn. 3:5).

KICHWA KIMOJA/MFALME MMOJA-KRISTO

Kanisa ni Mwili wa Kristo na Kristo peke yake ndiye kichwa (Efe. 1:22-23; 4:4). Ana mamlaka yote (Mt. 28:18; Kol. 1:18). Hajawahi kutoa mamlaka haya kwa mtu mwingine yeyote kamwe. Kwa kuwa Kristo ndiye kichwa, tunapokea maelezo yote kutoka kwake. Kwa kuwa yeye ni mfalme, ni lazima tumtii (Efe. 5:24).

Kanisa halina makao makuu duniani. Makao makuu ya Kanisa la Kristo yako Mbinguni. Kila kusanyiko la mwili wa Bwana liko huru na linajitawala lenyewe. Hakuna “Papa”, diwani, baraza wala kikundi cha watu kinacho-aongoza makusanyiko yote ya mwili wa Bwana.

WAZEE

Wazee wanachaguliwa katika kila kusanyiko (Mdo. 14:23; Tit. 1:5). Katika Agano Jipya, pia wazee wanaitwa waangalizi (Mdo. 20:28; 1 Pet. 5:2) maaskofu (Filp. 1:1; 1 Tim. 3:2) wachungaji (Efe. 4:11,12) wasimamizi (1 Pet. 5:1-4). Neno “mchungaji” ni sawa na “msimamizi” katika Agano Jipya wahubiri hawaitwi wachungaji kamwe. Katika kila kusanyiko, wazee waliopo ndio wachungaji (wasimamizi) wa kusanyiko hilo (kusanyiko hilo) 1 Pet. 5:1-4.

Sifa za wazee zimeorodheshwa katika 1 Tim. 3:1-7 na Tit. 1:5-13. Kwa nyongeza ili awe Mkristo mwaminifu, mzee ni lazima awe mwanaume mwenye mke mmoja na watoto waaminio. Asiwe mtu aliyeongoka karibuni. Vilevile katika kila kusanyiko kuwe na wazee zaidi ya mmoja. Maana Biblia inasema “wazee” (katika wingi) Mdo. 14:23; 20:17, 18, 28. Wazee wanatakiwa waliongoze, walilinde na kulilisha Kundi la Mungu. 1 Pet.5:1-4; Mdo. 20:28; 1 Tim. 5:17; Ebr. 13:17. [Yaani wafundishwe neno kwa usahihi].

MASHEMASI

Mashemasi wachaguliwe katika kila kusanyiko (Filp. 1:1). Sifa zao zimeorodheshwa katika 1 Tim. 3:8-13. Kazi ya mashemasi inajumuishwa pamoja na ile iliyoandikwa katika Mdo. 6:1-6.

Tena wanaostahili kuwa mashemasi ni wanaume tu. Wanawake hawana sifa za kuwa mashemasi kwa sababu hawawezi kuwa “mume wa mke mmoja,” 1 Tim.3:12.

WAHUBIRI

Wahubiri wana wajibu wa “kuhubiri neno” (2 Tim. 4:1-5). Kama wazee na mashemasi walivyo, pia wahubiri ni wanaume (1 Tim. 2:8-15). Wao ni waenezaji wa Injili, wahudumu wa neno la Bwana (2 Tim. 4:5). Katika Agano Jipya wahubiri hawaitwi kwa vyeo kama vile “mchungaji,” “mashemasi,” “dokta,” au “baba” Mt. 23:8-12.

WASHIRIKI

Mtu yeyote aliyeikubali Injili ni mshiriki wa Kanisa la Bwana (Gal.3:27; Efe. 1:3). Washiriki wa Kanisa wanawasikiliza wazee (Ebr. 13:17). Ni wajibu wao kuwafundisha waliopotea (Mdo. 8:4; 2 Tim. 2:24, 25). Inawapasa waenende katika “dini iliyosafi” (Yak. 1:27).

Uongozi wa Kanisa la Bwana unafanyika na Wanaume wenye sifa zinazostahili. Iwapo Kanisa halina muundo wa namna hii, haliwezi kuwa Kanisa alilolijenga Yesu. Kristo ni kichwa cha Kanisa lenye muundo wa maandiko tu. Kama Kanisa ulilopo lina wazee wanawake, mashemasi wanawake au wahubiri wanawake, basi hilo kanisa haliwezi kuwa lile lililojengwa na Yesu.

MWANDISHI: JOHN GRUBB